

MKATABA WA KUKODISHA (KIWANJA)

ENEO LA UWAZI

Mkataba huu umetiwa saini leo tarehe 27th ya mwezi July mwaka 2024

KATI YA

KAMPUNI YA YIFACOM, S.L.P 195I, LEMELA-MWANZA (Ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama Mkodishaji / Mmiliki)

NA

KAMPUNI YA FLOREGINE COMPANY LIMITED, S.L.P 32272, DAR ES SALAAM (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama Mkodishwaji/Mpangaji)

Ya kwamba, Mkodishaji ambaye ni mmiliki halali wa kiwanja Na. 19 Block B Kilichopo Mtaa wa Igekenaja ameamua kwa hiari yake mwenyewe kukodisha/ kukipangisha kiwanja hicho kwa Mkodishwaji ili akitumie kufanya shughuli zake za Magari kama vile:-kutengeneza magari (garage), kuhifadhi magari (packing) na kuosha magari (car wash) kwa mapatano/masharti yafuatayo.

1. Kwamba, mkataba huu ni wa miaka mitatu (miezi thelathini na sita tu) ambapo ni kuanzia tarehe **01** mwezi **08** mwaka **2024**.
2. Kwamba, mpangishaji/mmiliki anamkodisha mpangaji eneo hili kwa makubaliano ya kwamba, mpangaji atafanya maboresho ya kisasa katika eneo hilo/ au mazingira hayo ikiwa ni Pamoja na kuendana na teknolojia ya kisasa inayoendana na biashara hiyo ya magari ikiwa ni kama malipo ya upangaji wa eneo hilo ndani ya miaka mitatu.
3. Kwamba, kabla ya kumalizika kwa mkataba huu, kila upande una haki ya kuendelea au kutoendelea na mkataba mwingine. Taarifa itolewe kwa maandishi ndani ya siku 30 kabla ya kumalizika kwa mkataba huu.
4. Kwamba, baada ya muda wa upangaji kuisha mpangaji haruhusiwi kutoa kitu chochote kilichoengwa kiwanjani hapo.
5. Kwamba, mpangaji haruhusiwi kufanya biashara ya aina yoyote mbali na malengo ya mkataba huu, kufanya biashara ya aina nyingine ni kukiuka makubaliano ya mkataba.

6. **Kwamba**, mpangaji atawajibika kulipa kodi / madai yanayohusika na shughuli zake za Magari kama maji, leseni ya biashara n.k. Mpangaji hatahusika na gharama zinazohusika na umiliki wa kiwanja.
7. **Kwamba**, mmiliki atawajibika na ulipaji wa kodi zote zinazohusiana na umiliki wa kiwanja.
8. **Kwamba**, kila upande una wajibu wa kutunza na kuheshimu makubaliano haya. Kuvunja/ kukiukwa kwa kipengele chochote cha Mkataba huu kutasababisha kuvunjwa kwa mkataba huo.
9. **Kwamba**, mpangaji aangalie usafi wa kiwanja, ofisi, choo na mazingira ya kiwanja chote kama mifereji ya maji, utupaji wa taka ovyo. Kutofanya hivyo ni kukiukwa kwa mkataba huu.

KWA KUTHIBITISHA MAKUBALIANO HAYA: Pande zote mbili zinaweka Saini katika mkataba huu kama inavyoonekana hapa chini:-

Jina la Kampuni

YIFACOM COMPANY LIMITED



Tarehe

29/07/2024

Jina

FLOREGINEE COMPANY LIMITED



Sahihi

Tarehe

29/07/2024

MBELE YANGU:-

Jina: EZEKIEL JAMES

Saini: James

Cheo: WAKILI

Tarehe: 27th July 2024

